* CHECK FOR KILUGHA, COMPLETE TRANSCRIPT IN SWAHILI, TAPE #260-261

260 COMPLETE

{TAPE # 260, DONE BY NYAMUSI MAGATTI, AUGUST 2OO9}

{SIDE A}

Jan: kwahiyo wewe jina lako kamili?
George: naitwa George Wambura Rihamba
Jan: George nani?
George: kwa jina la nyumbani George Wambura
Jan: haha
George: Gehamba
Jan: Gehamba nani?
George: Gehamba Siwa
Jan: Siwa nani?
George: Siwa Gehamba tena
Jan: ni Rihamba au Gehamba?
George: Gehamba
Jan: Na Gehemba?
George: sasa hapo siwezi nikajua
Jan: sawasawa na ekehita yako?
George: mraji
Jan: na kwa sega ni upande gani?
George: mchapani mkihoja
Jan: na wao walifanya saro ni mwaka gani?
George: eeh hamsini na tano
Jan: haha na hii ni upande wa wasahi, warumaranja, bungerati?
George: wasahi
Jan: sawasawa na kwa rikora pia ni, ulifanya rikora?
George: eeh rikora mimi sikuishi katika maisha ya hapa nilikuwa mtumishi nilikwenda huko nikiwa kijana wa miaka ishirini na tano, nikatoka nyumbani kuwa mtumishi wa serekali
Jan: sawa au labda unipe historia hiyo, ulizaliwa lini?
George: nilizaliwa 1937
Jan: ulizaliwa wapi?
George: nilizaliwa Ikoma mtaa wa Mabokochabi
Jan: sawa ni wapi ukitoka Robanda ni?
George: Mgiroho [interruption]
Jan: haya katika maisha yako uliwahi kufanya nini na nini?
George: katika maisha yangu mimi mwaka hamsini na saba baada ya kuwa kijana wa miaka ishirini na tano nikaenda kutafuta maisha yangu Mwanza eeh nikaenda nikatafuta maisha yangu niakenda nikapata kazi kule, nikapata kazi shamba boi
Jan: shmaba boi ina maana gani?

George: mpishi aah hapana kijana wa bustani
Jan: kwa nani?
George: alikuwa mzungu mmoja alikuwa Kisimba Mwanza anaitwa Kwanza
Jan: haha
George: ilikuwa ni kisiwa Mwanza, mwaka hamsini na nane mwezi wa desemba
Jan: haha ulikaa huko sana?
George: nikakaa huko mwaka hamsini na nane huo ukaisha huyu bwana akaenda likizo ulaya na mimi nikarudi nyumbani Rubanda mpaka hamsini na tisa sasa januari, nikakaa hamsini na tisa hiyo mpaka hamsini na tisa mwezi wa tano akasema atakuja Mwanza tukutane Mwanza, nikatoka Robanda nikaenda Mwanza nilipofika Mwanza alikuwa kwa rafiki yake akasema huyu sasa hawzi kuja hapa mpaka aende Dar es salaam kwahiyo ukae hapa siku nne na baada ya siku nne akishafika kule lakini hajapata nyumba yake binafsi kwahiyo subiri siku nne hapo akishapata nyumba yake ya binafsi basi ndiyo utakwenda, nikakaa mwanza siku nne mwezi wa tano huo basi mwezi wa tano huo tarehe tisa basi akapiga simu, nikaondoka Mwanza kwenda Dar es salaam
Jan: haha
George: nilipofika Dar es salaam nikakuta huyu bwana ameshafika akanipokelea stesheni tuakenda kwenye nyumba yake binafsi, niakendelea kufanya kazi kwake, kazi yangu ileile
Jan: ya bustani?
George: eeh mtunza bustani na kufua nilikuwa nafua nguo, nikakaa pale tangu hamsini na tisa hiyo mpaka sitini na nne januari nikaacha kazi hiyo nikaingia jeshini
Jan: haha kwanini uliamua kwenda jeshini?
George: eeh tulipata mwito wa baba wa taifa Julius Kambarage Nyerere kwamba tulitaka kuunda jeshi la wananchi ya Tanzania, kuunda jeshi mpya sasa jeshi la wananchi, kwasababu kulikuwa na jeshi la waingereza sasa tulitaka kuunda jeshi la wananchi ya watanzania kwahiyo nikafuata wito huo, eeh nikakubaliana na bwana yule akasema basi nenda jeshini, nikaenda nikajiunga, kwanza kwenda jeshini nikaanza na National Service, tarehe mbili mwezi wa pili, nikafanya hapo januari hiyo mpaka tarehe moja mwezi wa sita nikaingia jeshi
Jan: haha sawa halafu
George: tukaingia jeshi tarehe moja mwezi wa sita mpaka tahere moja septemba tukamaliza mafunzo ya jeshi, tukagawiwa kwenye vikosi sasa, mimi nikaperekwa kusini mwa Tanzania, nikakaa kule, tukaenda kufanya ulinzi katika kusini mwa Tanzania, tukaaa huko mwezi wa kumi tulikwenda Chingwea, nikakaa pale mpaka sitini na nane mwezi wa tatu nikaja Dar es salaam
Jan: ulikuwa bado kuoa?
George: aah nilioa Chingwea baada ya miaka mitatu, sitini na saba nilioa
Jan: haha ni mke wa hapa au wa huko?
George: wa hapa
Jan: kwahiyo ulirudi nyumbani uka..?
George: nikaja likizo nikaja nikaoa halafu nikaenda naye kazini sasa
Jan: haha anaitwaje?
George: anaitwa Rista Nyamasagare
Jan: sawa haha ulirudi tena Dar es salaam

George: aah ilikuwa bado sitini na saba, nilipooa nilikuwa bado Machingwea nikarudi huko, sitini na nane nikahamia Dar es salaam sasa kule nilikaa miaka mitatu, Dar es salaam nimekaa mkapa sabini na moja halafu nikahamia Tabora
Jan: mmh sawa
George: nikakaa mpaka sabini na tano nikarudishwa tena Dar es salaam kituo cha Maswa cha jeshi, sehemu moja inaitwa Kurasini, kipindi hicho sasa nilishakuwa koplo wa jeshi na mimi nilikuwa dereva
Jan: sawa
George: nikakaa sabini na tano hiyo Kurasini sabini na saba januari nikahamia Kigamboni
Jan: mmh sawasawa
George: nikakaa Kigamboni sabini na saba hiyo, mwaka moja tu, sabini na sita nikaenda kule Makoma Dar es salaam hapohapo
Jan: haha sawa
George: pale nikakaa sabini na saba mpaka themanini na moja nikahamia Mwanza Nyegezi, pale nikakaa mpaka themanini na nane nikahamia hapa kwetu Ikoma
Jan: mmh sawa
George: eeh kwahiyo nikahamia hapa Ikoma themanini na nane, nikakaa mwaka moja tu, themanini na tisa nikaenda kule (not clear), nikakaa themanini na tisa mpaka tisini niakrudishwa Boti mpaka tisini na mbili nikaenda Chiabakari
Jan: mmh kwa kazi gani hapo?
George: hiyo hiyo kwenye kikosi
Jan: haha
George: tisini na nne nikastaafu kazi sasa desemba
Jan: haha sawa halafu ukarudi tena?
George: eeh nikarudi nyumbani
Jan: sawasawa na watoto una watoto wangapi?
George: watoto nina mmoja
Jan: sawa haya labda twende kwa mzee mwingine

Jan: jina lako?
Samweli: Samweli Mbuya Mongita
Jan: na Mongita ni wa nani?
Samweli: Mwishagori
Jan: na Mwishagori?
Samweli: Mwokibeni
Jan: haha Mwokibeni?
Samweli: ni mwisho
Jan: aah sawasawa na kwa ekehita?
Samweli: mrati
Jan: na kwa warati ni upande gani?
Samweli: busahi
Jan: busahi haha na saro yenu ilikuwa ni nini?
Samweli: ni moja
Jan: kwahiyo mlikuwa pamoja?

Samweli: eeh sisi wote ni rika moja
Jan: haha hamsini na?
Samweli: na tano
Jan: haha sawasawa ulizaliwa lini?
Samweli: thelathini
Jan: kwahiyo unamzidi kidogo
Samweli: eeh namzidi
Jan: ulizaliwa wapi
Samweli: Ikoma kule kijiji cha Mwani, mtaa ule unaitwa Mwani
Jan: ni karibu na hapa?
Samweli: eeh karibu na barabara ya zamani ya kwenda Sibora huko
Jan: haha
Samweli: [kilugha]
Jan: kwahiyo katika maisha yako labda ueleze ulikuwa unafanya nini?
Samweli: mimi baada ya kukaa nyumbani nikaenda jeshi ya Musoma Rubanda, niliendelea na hiyo mpaka arubaini na sita, bikaacha nikarudi arubaini n asaba nikakaa nyumbani mpaka mwaka hamsini na moja niliondoka nyumbani nikaenda Mwanza
Jan: haha
Samweli: Mwanza nimefanya kibarua katika mashine ya kusindika brashi, halafu nikatoka Mwanza mwaka hamsini na mbili nikaenda arusha nilikuwa natafuta kazi tu kutafuta maisha sasa Arusha mwaka hamsini na mbili nikaingia katika kikosi cha polisi
Jan: sawa
Samweli: jeshi la polisi nikaenda Dar es salaam kwenye mafunzo, mpaka mwezi wa tisa nikamaliza mafunzo ya polisi
Jan: haha hamsini na?
Samweli: hamsini na mbili
Jan: haha
Samweli: halafu nilipomaliza nikaperekwa Tanga, nikakaa huko mpaka hamsini na nne nikaenda Korogwe, Korogwe kule nikakaa mpaka hamsini na tisa, lakini kabla ya hapo hamsini na nane nilirudi nikaoa
Jan: haha
Samweli: nikaoa Anna Mekaba, sitini tukapata mtoto wa kwanza huko Korogwe
Jan: aah sawa
Samweli: mwaka sitini na mbili nikahamia Mwanza nikiwa katika hii idara ya polisi, sitini na tatu nikahamia Tarime mpaka sitini na saba mwezi wa sita nikahachishwa kazi, sabini na nne (not clear too much background noise) nimekuwa hapa mpaka sasa
Jan: mmh kwanini uliamua kwenda Nyachoka badala ya kurudi Robanda?
Samweli: aah hapana sasa ile ilikuwa ni ihari ya mtu
Jan: aah
Samweli: eeh ihari ya mtu, wakati huo kwetu tulikuwa tumekwishahama kutoka Robanda tulikuwa Isenye, sasa niakona nirudi karibu na.. (not clear)
Jan: na ulikuwa unavutwa na kitu Fulani huko ambayo uliona ni mahali pazuri uende kukaa?
Samweli: (not clear) karibu na barabara (not clear) walipohamisha vijiji vya jamaa wakapabomoa nikaja hapa sasa

Jan: aah sawa
Samweli: nikaenda nikajenga barabarani
Jan: aah sawasawa sasa naona nyinyi wote sehemu kubwa ya maisha mlikuwa nje kwa kufanya kazi hii wakati ule ilikuwa kawaida wengi walitoka au nyinyi mlikuwa tofauti na wengine?
George: aah wengi vijana walikuwa wanatoka inategemea na mtu unapopendelea unajua mtu ukishakuwa mkubwa kidogo unataka utafute maisha yako, maana sasa huwezi kukaa unawategemea wazee, ukishakuwa mkubwa na miaka ishirini kuendelea mpaka ishirini na tano kuendelea unataka utafute maisha yako upate kazi ufanye, uoe, upate watoto, uwe katika mji wako wewe binafsi
Jan: kwasababu uliona mzee alikuwa hana ng#ombe wa kutosha?
George: aah mimi mzee wangu alikuwa ana mbuzi, kwahiyo nikaona nijitafutie maisha ya kupata pato ili nijisaidie katika maisha yangu
Jan: hata wewe uliona baba hakuwa..
Samweli: hata mimi, baba hakuwa na mali ya kuweza kunitosha kwahiyo niliona nitafute mali niweze kuoa
Jan: haha
Samweli: anilipokuwa huko nikanunua mifugo nikaoa
Jan: na ulipoona hasa hawa ambao baba hakuweza kuwasaidia ambao walitoka kufanya kazi au hata?
Samweli: aah hapana alikuwa anawasaidia tu
Jan: haha
Samweli: wengine wanasaidina, wale wadogo unawatunza
Jan: sawa hata baba zenu walikuwa wanaenda nje kufanya kazi?
Samweli: eeh wengine walikuwa wanaenda
Jan: kwa mfano baba yako alienda kufanya kazi?
Samweli: hata
Jan: na yako?
George: mimi vilevile hakwenda
Jan: aah
George: mimi baba yangu hakwenda alikuwa anafanya kazi ya kilimo tu, analima chakula, akipata chakula labda anauza mbuzi anauza ng#ombe ndiyo ilikuwa kazi yao lakini kazi ya kwenda nje kulikuwa hakuna ilikuwa ni hapahapa, kazi ilikuwa ni kulima tu, akipata mazao anauza na kupata mahitaji
Jan: au waliwahi kufanya biashara huko sukuma baba zenu?
George: eeh biashara walikuwa wanafanya lakini biashara na wasukuma walikuwa wanafanya biashara ya wanyama
Jan: ya wanyama pori?
George: kwasababu sisi ni wawindaji, sasa walikuwa ikifika mwezi wa sita wameshamliza kuvuna, sasa ni kiangazi mwezi wa sita mpaka mwezi wa kumi na mbili walikuwa wanakwenda kuwinda kwenye mapori wanakwenda kule kuwinda wanyama wanapata wanyama na ile mikia ya nyumbu basi wanapereka usukumani, wanakwenda zile nyama wanauza wanaweza kupata mbuzi na ile mkia wa nyumbu wanauza vilevile wanabadilisha wanapata labda ndama kama moja, labda na mikia mimi nina tati huyu ana nne basi ile mkia tunabadilisha ng#ombe. Huyo

ng#ombe tunamchangia tunakuja naye nyumbani na mbuzi tunakuja nao nyumbani sasa tunamlisha sasa akizaa tunaweza tukagawana, akizaa mtoto wa kwanza anachukua huyu, labda akizaa mtoto wa pili anachukua huyu sasa mimi nabaki na yule, ndio biashara ilikuwa inafanyika na tumbaku vilevile hapa walikuwa wanapereka tumbaku sukuma sana
Jan: haha
George: kwa kutumia sigara, wananusa
Jan: haha kwahiyo ilikuwa hasa kazi ya akina baba zenu ambao walienda sukumani, ikifika rika yenu mlikuwa mnaenda sukuma au hapana?
Samweli: ilikuwa kama sisi#
George: wengine baadhi yetu, rika yetu walikuwa wanakwenda, ila ambaye hakuwahi kwenda kutafuta makazi kwenye miji walikuwa wanaenda
Jan: haha na hata kabla ya tuseme wakati wa babu walikuwa wanafanya nini ili na wao wapate mali?
George: babu zetu waliozaa baba zetu?
Jan: mmh
George: wale walikuwa ni kulima, walikuwa wanalima sana, sisi wa Ikoma zao letu hasa ilikuwa ni ulezi na mtama ndio zao kuu ilikuwa, walikuwa wanalima mashamba amkubwa ya ulezi na mtama, sasa wakishavuna kama una ulezi mwingi, na watu wote walikuwa hawapati chakula wengine hawawezi kulima, wengine labda..basi wanauziana, yule ambaye hana chakula basi analeta mbuzi anakupa wewe unapatia, labda kama ni ng#ombe anakupa ng#ombe wewe unampa chakula, ndio kazi waliokuwa wanafanya wanabadilishana, lakini kazi hawakwenda kutafuta, unajua babu zetu wazungu walikuwa hawajaenea sana, kwahiyo walikuwa wanafanya kazi hizi za kulima tu, kubadilishana ng#ombe, mbuzi wanauziana halafu mtu anapata mali anaoa na kuwinda
Jan: babu alikuwepo wakati wa wajerumani kufika?
George: eeh mimi sijui kama babu alikuwepo lakini babu mzaa mama alikuwepo maana walijenga hapa Foti kwasababu mama aliniambia akasema wajerumani walivyokuja mama alikuwa kama wewe wakasema wajerumani walivyokuja babu akajenga Foti basi walikuwa wawili
Jan: baba
George: babu yangu mzaa mama, wanakimbia kumpokea, alikuwa ananihadithia mama
Jan: walikuwa huko karibu na Foti
George: eeh walikuwa Robanda pale, ukitoka Foti ukivuka mto basi maeneo yale ndio walikuwa, kwahiyo wale wazee walikuwa wanajenga Foti jioni wanakuja nyumbani
Jan: inawabidi kila mtu aende kuwasaidia kujenga ilikuwa lazima?
George: wale walikuwa wanashikwa na watemi, si walikuja wakaweka watemi sasa wale watemi walikuwa wanapita kwenye miji, wakipata vijana kama hawa wapo basi wanasema wewe na wewe basi mnakwenda kujenga boma, wale vijana ndio walikuwa wanakwenda kujenga
Jan: haha unajenga kwa siku Fulani halafu unatoka tena?
George: aah walikuwa wanajenga tu, hiyo ikiisha wanakwenda kupigana
Samweli: tuseme wale walipofika waliamua kujenga ile boma, wakishajenga tayari wamemaliza kazi imeisha lakini walijenga
Jan: na walisumbua sana watu kushika wajenge?

Samweli: unajua wale walipofika pale illikuwa matatizo maana wale waliokuwa wanajenga lazima wajenge kwa nguvu kwasababu ile ilikuwa ni kikosi ya jeshi, walikuwa wakali sana wa Ikoma hawasikii Kiswahili basi ikawa wanasumbuanasumbuana lakini baadaye wakishaelewana walipokwishajenga wakaona ni afhadali
Jan: na katika enzi za babu uliwahi kusikia kwamba walipata njaa kubwa sana au ulisikia kwa babu?
Samweli: njaa iliwahi kutokea mwaka moja, mimi bibi yangu mzaa mama alisema ilikuja njaa kubwa sana sijui ni mwaka gani
Jan: ilikuwa inaitwaje hiyo njaa
Samweli: walikuwa wanaita njaa ya miguu maana yake waliugua miguu [kilugha]
Jan: agecha magora sawasawa
Samweli: sasa walikuwa wanasema agecha magora walikuwa wanajitahidi sana, chakula kilikuwa kinapatikana usukumani unajua wasukuma sisi tulikuwa tuna uhusiano mzuri, tulikuwa na mazoea, sasa mtu kama alikuwa na uwezo wa kuhama anaweza kuondoka akaenda usukumani kutafuta chakula kuletea watoto na wengine..
Jan: walikaa kabisa
Samweli: walikwenda wengine walikaa huko moja kwa moja
Jan: kwa miaka
Samweli: mpaka leo wanakaa huko huko, wakageuka kuwa wasukuma na wengine wakarudi na wengine hata walikuwa wanaooza watoto wanapata chakula
Jan: haha pia walipereka wanyama pori huko kubadilisha ili wapate chakula au hii bado wakati wa njaa?
Samweli: aah hiyo ilikuwa bado, hiyo ilikuwa ni kabla ya hapo
Jan: lakini walipokuwa huko wakaona kwamba kumbe wasukuma wanapenda mikia?
Samweli: eeh wasukuma wanapenda mikia, eeh kwasababu wale mabinti wa kisukuma walikuwa wanaita kama#

[THE END OF SIDE A]

[SIDE B]

Samweli: wanashika halafu wale mabinti wa kisukuma walikuwa wanapenda, sasa ni umaridadi sasa wanakwenda kucheza ngoma, ilikuwa ni sifa yao umaridadi walikuwa wanavaa na kuchezea ngoma sasa hawa walipojua wakazidisha sana kuwinda kwenda kuuza wapate biashara
Jan: na wao walioenda kufanya hii biashara ya udodi wakatajirika wakapata ng#ombe wengi au si sana?
Samweli: si sana, ilikuwa kadri tu
Jan: haha kwahiyo hakuna kipindi unaweza kusema wa Ikoma walikuwa na ng#ombe wengi sana au ilikuwepo ?
Samweli: walikuwa na ng#ombe wa kiasi isipokuwa miaka ya karibuni walikuja kuwa mbuzi wengi kuliko ng#ombe, walikuwa na mbuzi wengi sana, unakuta mtu ana mbuzi sabini wanalala kwenye manyumba tatu, zamani hasahasa ilikuwa ni kilimo

Jan: ni akina nani?
Samweli: babu zetu na baba zetu ndio waliendelea kutajirika hawakuwa na matatizo
Jan: mmh na naona nyinyi wote mlipoenda kufanya kazi jeshhi na polisi hii ni kawaida kwa wa Ikoma wanapenda kazi ya aina hiyo?
Samweli: hapana kuna wengi walifanya kazi za aina mbalimbali kuna wengine walikwenda tuseme ni kila mtu alichobahatika kupata
Jan: lakini si kweli kwamba jeshi wengi wanatoka mkoa wa Mara?
Samweli: wengi wanatoka mkoa wa Mara
Jan : kwanini ?
Samweli : watu wa mkoa wa Mara wana nguvu sana kwahiyo jeshi wanapenda mtu mwenye nguvu hawapendi mtu mvivu
Jan : haha
Samweli : wanasema ni mtu fiti, sasa mtu mvivu jeshi haitaji sasa watu wa mkoa wa Mara ni watu wenye nguvu ya kufanya kazi, vijana wana nguvu sana ya kufanya kazi kwahiyo wazungu wakawapenda
Jan : aah kumbe au hii inatokana na kazi ya huko porini kuwindawinda walikuwa tafu sana au inatokana na nini ?
Samweli : pamoja na hiyo kazi lakini vilevile maumbile yao ilikuwa ni ngumu ya kufanya kazi porini, kulima , kwahiyo kazi zao ilikuwa ni kazi ngumu kwahiyo kama wewe unazaa mtoto unapata anapenda kazi ya baba yake na mama yake, hata kijana wangu alikuwa askari
Jan : kwahiyo hata leo wengi wa jeshi wanatoka mkoa wa Mara?
George : hapana hata mikoa mingine lakini percentage kubwa inakuwa mikoa ya huku
Jan : mmmh na zamani hapa mlikuwa na hizi machimbo kama Buhemba au Nyegoti wengi waliwahi kufanya kazi hiyo au hawakupenda hii kazi ya machimbo ?
George : aah walifanya mpaka Kilimafedha walifanya, baba zetu walifanya, na baadhi ya rika letu waliotutangulia wao walifanya Buhemba, Kilimafedha
Jan : kwahiyo sio kwamba watu walikataa kazi ile ya machimbo ?
George : aah hapana
Jan : waliona ni sawa?
George : eeh wailifanya kuwapatia manufaa, wakapata hela wakanunua mbuzi, wakanunua ng#mbe wakaoa
Jan : au kwenda mpaka Magadisoda walienda?
George : eeh walienda
Samweli: walikuwa wanakwenda kwa miguu sasa
Jan : haha
Samweli: sasa rika yetu hiyo hasa wakubwa wanaotuzidi kidogo walienda sana Magadisoda
Jan: haha na Nairobi
Samweli: eeh na Nairobi
Jan: haha
George : rika yetu wale wakubwa sasa
Jan : walipenda sana sehemu hiyo?
George : walipenda sana, hata Magadisoda wengi walikwenda
Jan : kwanini walipenda hiyo?

George : eeh kazi ilikuwa inapatikana kule na wenyewe wanapenda kufanya kazi ili wapate maisha mazuri kwahiyo wakisikia mtu labda amekwenda amefanya kazi amerudi wanakuja na hela wananunua mbuzi basi na mtu mwingine anapenda basi wakawa wanakwenda kwa mwamuko huo
Jan : haha na ninyi mnavyoona vijana wa siku hizi mnaona na pia wao wana nguvu ya kwenda kupata kazi na kurudi na mali au?
George : wanaweza lakini sasa hivi ndio kazi haipo, zamani ilikuwa kazi si ya kutafuta sana ukienda ukitafuta kazi tu unapata lakini sasa kazi zimekuwa chache
Jan : haha
George : wanapenda wafanye lakini kazi hayapo
Jan : kwahiyo imekuwa ni shida kuliko wakati ule ambao..
George : ukienda unapata tu mkienda kama watu kumi mnakwenda Magadisoda wote mnaingia
Jan : wote mnapata?
George : mnapata, ilikuwa si rahisi mtu kwenda kutafuta kazi ukakosa ukarudi nyumbani
Jan : na malipo yalikuwa ni mazuri?
George : si mabaya sana
Samweli: mimi nilipoanza kufanya kazi, ya kwanza kabisa ilikuwa hamsini na sita nilianza kwa shilingi sita
Jan : kwa mwezi
George : eeh kwa mwezi
Jan : lakini iliweza kununua vitu vingi?
George : aah shilingi mbili ulikuwa unanunua mbuzi, halafu baadaye nilipokwenda Mwanza mwaka hamsini na saba ndio nilianzia mshahara wa shilingi sitini, hapo ikawa imeshapanda kidogo
Jan : naona imepanda sana, mara kumi
George : eeh shilingi sitini
Samweli: mimi nilipoanza kazi ya polisi depo kwenye mafunzo nilikuwa Napata shilingi sitini na moja
Jan : haha
Samweli: natoka depo Napata shilingi mia na mbili, zilikuwa zinatosha
Jan: hata kutuma nyumbani zingine unatuma?
Samwel: natuma, ukitumba shilingi mia mbili wananunua karibu ng#ombe tatu
Jan : ooh ok, kwahiyo mnaona maisha ya siku hizi ni ngumu kuliko wakati ule?
SamwelI: inalingana kwasababu ya wakati, wakati huu ukiwa na shilingi laki moja zamani ulikuwa kama laki moja, ulikuwa na mia mbili zamani ni kama laki moja
Jan: haha na nyinyi wote mlianza kuwa watu wazima wakati wa uhuru ilipoingia?
Samweli : uhuru imenikuta kazini
Jan : na nyinyi mmewahi kufanya kazi katika chama cha TANU au kwa kugombania uhuru au?
Samweli : tulijaribu kidogo, mimi nimeingia chama cha TANU hamsini na tisa baada ya miaka miwili, sitini na moja tukapata uhuru, sasa wakati tulikuwa vijana miaka ishirini na tano, ishirini na tatu
Jan : mkafanyaje ili mpate?

Samweli: mimi kwa upande wa polisi hatukuhurusiwa, haikuruhusiwa askari kuwa mwanachama mpaka baada ya uhuru sitini na nne mwezi wa nane ndipo serekali ikaamua askari polisi wanaweza kuingia chama, nikaingia sasa chama kule Tarime
Jan: lakini nyinyi mlikuwa kwenye siasa ambayo mlitaka mpate uhuru na nini?
Samweli: ndio tulikuwa tunapenda tupate uhuru, tulipoingia ile chama, huyu sasa alikuwa mbele yangu yeye alishakuwa askari mimi nilikuwa raia nilikata kadi ya TANU, sasa ilikuwa ile kadi ya TANU unalipa kwa kila mwezi ulikuwa unalipa senti hamsini, tulikuwa na kadi mbili kadi ya vijana na kadi ta chama ya TANU, kwahiyo ulikuwa unalipa senti hamsini kila mwezi ya kuchangia chama
Jan : na uliwahi kusikia Nyerere anapoongea?
Samweli: eeh nilisikia, mimi mwalimu Nyerere nilimuona mwaka hamsini na tano mara ya kwanza kabisa alikuja Robanda alitokea Arusha akaja akalala kwa chief Rihoja, ndio siku ya kwanza nilimuona mwalimu Nyerere, nilikuwa mdogo tu sijaenda kufanya kazi yoyote
Jan: haha na mlipokuwa wadogo mlipata chief wa Ikoma alikuwa nani?
Samweli: sisi tulipoanza wajani yani kujua alikuwa chief Nyambehu
Jan: haha yeye alianza lini kuwa chief?
Samweli: hiyo siwezi kujua kwasababu tulikuwa wadogo, siwezi kujua ilikuwa mwaka gani, mimi nilipoanza kuingia shule yeye alikuwa chief
Jan: na baada ya Nyambehu alikuwa nani?
Samweli: akawa Machabe kijana wake
George : akawa Machabe Nyambehu
Samweli: Nyambehu alikaa mwaka moja arubaini na tano hiyohiyo akawa ameharibu akafanya makosa akawekwa chief Marasi
Georrge: Marasi ndio akawa chief
Jan : halafu akakaa?
George : akakaa mwaka mmoja akafariki sasa wakamweka kijana wake anaitwa Machaba Marasi
Jan : akakaa yeye sana?
Samweli: mpaka sasa uhuru umemkuta, ndio wanasema mwalimu alikuja akakaa kwake pale Rubanda hamsini na nane
Jan: babu zenu waliwaambia walivyochagua chief wa kwanza kwa wa Ikoma wakampataje?
Samweli: {kilugha}
George: wa kwanza ndio huyo ulikuwa unamsikia
Jan : kwa wajerumani
George : eeh
Jan : na ulisikia walimpataje au hukusikia hiyo historia?
George : walikuwa wanakuja wanasema kwamba wanapendekeza majina sasa wanawasimamisha sasa wanasema huyo mtu ambaye wanampenda awe chief basi wewe unasimama, na mwingine anasimama basi atakayekuwa na wingi ndio anapta uchief
Jan : haha
Samweli: wazungu wakija wakisema wanataka chief wanawaambia wa Ikoma, sasa wa Ikoma wanaitana milango yote wanakaa mkutano wanasema sasa nani tumweke uchief, sasa wa Ikoma wenyewe walikuwa wanajua mtu mwenye tabia nzuri anaweza akawawakilisha basi wanasema fulani

George : wanasema tena mwingine tena wanataja, labda majina mawili
Samweli: wanasema sasa nani anampenda Fulani, na nani wanampenda Fulani, basi kama wananipenda mimi wanasimama mgongoni mwangu na wanayempenda huyu wanasimama mgongoni mwake sasa wanahesabu, sasa yule akipata watu wengi ndiye anakuwa chief
George : ndivyo walivyochagua
Jan : na watu walikuwa wanawapenda machief ya wakoloni au wakaona wanalazimisha mambo mabaya?
Samweli: hapana walikuwa wanachagua ni watu wao, maana wanapomchagua huyu
George : aah wenyeji walikuwa wanawapenda
Samweli: maana walikuwa wanamchagua mtu wa kabila yao sasa walikuwa hawana matatizo naye halafu wanajua chief kazi yake anawaunganisha wale wenyeji na wakoloni anakuwa katikati kwahiyo anawaunganisha, kama mzungu anakuja kisiri anataka watu wafanye kazi gani na nini wanamwambia chief, chief anawaita watu wake anawaambia tunataka tufanye hiki na hiki na hiki, kwahiyo chief alikuwa anawaunganisha watu
Jan : lakini kama wakoloni wanawalazimisha wafanye kazi ambayo watu hawapendi si wanamkasirikia huyu chief wanaona huyu?
Samweli: hapana hawawezi wakafanya hivyo
George: wao wanasema waliokuwa wanawakasirikia ni wale wakoloni si chief wao maana amri imetoka kwa mkoloni
Jan : aah sawa maana nikisoma kwenye hii nyaraka za wakoloni wanasema kwamba kuna kipindi waliona kuna njaa huko Robanda wanataka watu walime mihogo lakini chief anakataa na wao wanasema kwanini hawataki kulima mihogo sasa niambie kwanini hawakupenda kulima hii mihogo
George : kwanza chief alikuwa anawaita akishapata amri anawaita wale wazee sasa anakaa nao anawaambia nyinyi mnaonaje, sasa wale wanasema nchi hata ukilima haiwezi ikastawi maana ilikuwa ni nchi kame, mvua ilikuwa chache
Jan : mmh kwahiyo anarudi kuwaaambia wakoloni hatuwezi
Samweli: anasema hii ardhi haistawishi mihogo
George : sasa akishawaambia mkoloni basi anasema hapana kwasababu ya njaa hii waambie lazima walime, basi wanalima, sasa wanalima ovyoovyo kwasababu ni kitu hakitastawi, wanalima ovyoovyo kwasababu wamelazimishwa
Jan : haha kama sikosei hii amri ya mihogo ilikuwa hata mwaka thelathini na kitu?
George :eeh
Samweli: hata arubaini na tano walileta wakaipanda lakini ikakataa, kila sehemu kitongoji kama hiki wanachagua mahala Fulani wanalima pamoja wanapanda hiyo mihogo
Jan : lakini haikustawi
Samweli: haikustawi kwasababu nchi ni kame, inaota lakini haitoi inakauka
Jan: mmh kwahiyo wakati wa njaa kama waliona mihogo haiwezi kuwasaidia walifanya nini ili kusaidiwa wakati wa njaa, ulivyowaona?
Samweli: walikuwa wanapata chakula kwa watu ambao walikuwa wamelima ulezi maana ulezi ilikuwa inakubali, walikuwa wanatafutatafuta chakula ya kuweza kuwasaidia
Jan: mmh kwa mfano miti gani?
Samweli: kwa mfano wanaita kitani wanachuma na kuna mboga Fulani na asali
Jan: na asali walikuwa wanapata wapi?

Samweli: walikuwa wanapata kwenye miti na kwenye vichuguu
George : wengine wanatengeneza mizinga
Jan : na kuwinda waliwinda zaidi wakati wa njaa?
George : wanyama ndio waliweza kuwasaidia
Jan : haha
Samweli: wanyama na wanyama za mifugo
Jan: wakaenda kuwabadilisha au wakala tu?
Samweli: za kula tu, na kubadilisha vilevile unaweza ukapata nyama kiasi labda tani kumi basi unakausha unabadilisha huko Ikizu , zanaki
Jan: kwahiyo wakati wa njaa huu uwindaji ikawa sehemu kubwa ya maisha yao?
Samweli: eeh ndiyo kwasababu anajua akipata nyama atapata chakula
George : sababu wakawa, ili waue kwa wingi wakawa wanachimba mashimo, wanchimba shimo refu, halafu wanaleta wanyama pale wanakufa wengi
Samweli: wakishajaa wale wengine wanakufa mle
George: kijiji kizima sasa kinahamia pale, zile nyama wanapereka nyumbani inakuwa ni sehemu chao ya chakula
Jan : haha na hii shimo zilikuwa zinaitwaje kwa Ikoma?
Samweli: riko
George : au obini
Jan : haha na waliua wengi ambao hata nyama hawakuweza kutumia au walitumia nyama zote?
Samweli: nyama waliweza kutumia kiasi, za kutumia na za kukausha
Jan: haha na nyingine?
George : hiyo wanakausha wanaweka kwenye maghala
Samweli: si ndio ilikuwa chakula
Jan : haha na hii ilikuwa wakati hata wa baba hata wa babu hata nyinyi?
Samweli: walikuwa wanaendelea, kuna miaka sio miaka yote iliyokuwa na njaa kuna miaka
Jan: hasa unaweza ukakumbuka ni miaka gani njaa ilikuwa kubwa?
Samweli: miaka ambayo mimi nilipokuwa mkubwa arubaini na tatu mpaka arubaini na saba ilikuwa njaa, hiyo ilisababisha hata ile shule ya Robanda ikasimama maana watu walihama kwa wingi
Jan: hata kwa miaka mine mitano inaweza kuwa
Samweli: njaa kabisa
Jan: njaa kabisa nini inasababisha hii?
Samweli: ni ukame mvua inakuwa chache, hiyo sehemu ya kwetu ni uwanda wa chini ndio maana wakati mwingine wakahamua wahamie hapa, maana hapa mazao yanastawi kama viazi chakula kingi zinastawi
Jan: lakini kabla ya miaka hiyo hii sehemu ya Rubanda ilikuwa ni pazuri tu?
Samweli: ni pazuri tu wakati mwingine kama inanyesha ni pazuri kama mvua haipo inakuwa shida
Jan: na mvua kawaida yake inaenda inakuja kwa kipindi chake?
George : eeh
Jan : kila baada ya miaka mingapi

Samweli: kila mwaka, maana Robanda wanaanza kulima desemba mpaka mwezi wa sita wanavuna basi mvua inakimbia mpaka desemba tena
Jan: lakini kawaida wanaweza wakahesabu kuna miaka minne nitano bila mvua tena inarudi kwa miaka?
Samweli: eeh
Jan: kwa miaka ngapi ambayo wanaona au hakuna?
Samweli: hakuna hesabu labda inaweza kuwa kwa miaka mitatu minne halafu ikawa neema tena kwa miaka tena minne, miwili
Jan: hamwezi kujua
Samweli: hatuwezi, haina kipindi maalum tangu tumekuwa sasa inakuwa hivyohivyo, miaka miwili inakuwa mizuri miaka miwili inakuwa tena ni shida tu
Jan: kwahiyo wanaangalia tu tuhame tusihame?
Samweli: aah sasa hakuna kuhama, sasa wakati huutuliopo sisi usafiri ni mzuri unaweza ukafuata chakula, kwahiyo hamna kuhamahama sababu wale walikuwa wanahama sababu hawana usafiri, walikuwa wantembea kwa miguu unatoka hapa labda unafuata chakula Tarime kwa miguu labda ikizu au Ikoma au zanaki maeneo hayo ndio walikuwa wanafuata chakula, Tarime, Ngorime, Zanaki, Ikizu na Sukuma kwahiyo kwas asa hivi hakuna shida ya kuhama sababu magari yako mengi, ukitaka kufuata chakula mwanza unafuata unakuja, hata Tarime au Arusha kinakuja
George : mara ya mwisho njaa iliyokuwa kali sana mwaka arubaini n asaba na arubaini na nane hiyo ndiyo ilifanya wa Ikoma wakatawanyika, wengine wakaenda Ikizu, wengine wakaenda usukuma
Jan : mmh aah kumbe na wakati ule serekali ilileta chakula vilevile?
Samweli: nakumbuka mwaka arubaini na tano bwana DC alikuja mpaka shuleni akamuuliza mwalimu kwanini watoto hawapo? Akasema ni shauri ya njaa, akasema je nikileta chakula wanaweza wakawepo, akasema ndio walileta lori nzima, halafu mzee moja akaleta chakula loris asa watoto wanapitia pale tunakula lakini vilevile kwasababu njaa ilizidi kuwa kali ikaonekana vilevile haikuwa dawa, wanasaidia watoto lakini wazee kule nyumbani ni njaa, mtoto aliyekuwa anakwenda kusoma anaweza kula, waliobaki nyumbani hawakuweza kula kwahiyo ikaonekana haikusadia sana
George : ikafika arubaini na nane wakawekwa wahindi pale, wanaleta unga wa mahindi ambao ilikuwa inaitwa reureu
Jan : ilitengenezwa na nini?
George : ilisagwa na mashine
Samweli: wakasaga chakula wakaleta mahindi pale kwa wingi mwenye uwezo ananunua, watu wakaenda na mifugo pale
George: kwahiyo mtu anauza ng#ombe yake ananunua reureu, ulikuwa ugali mtamu sana
Jan : na ninyi mnaweza mlipokuwa watoto mliona wa Ikoma wengi walikuwa wanakaa karibu na robanda pale au walikuwa kwenye sehemu zingine?
Samweli: walikuwa sehemu nyingi
Jan: sasa taja sehemu ambazo walikuwa wanakaa?
Samweli: kulikuwa na sehemu moja ilikuwa inaitwa Mrago
Jan: Mrago ni wapi
Samweli: ni magharibi sana ya Robanda, mito ilikwenda kukutania pale, walikuwa wanakaa pale

George : wengine walikuwa wanakaa Masaka
Jan : Masaka ambayo iko?
George : ipo kusini mwa Robanda
Samweli: kusini mashariki
Jan : na hawa wote ni wasahi au hawa ambao wanakaa Mrago?
George : hao wanakaa Mrago
Samweli: Mrago walikuwa wanakaa wangerati
George: eeh Mrago ni wangerati
Jan : haha na Masaka?
George : Masaka walikuwa wanakaa warumaranja
Jan : haha
George : yani abaranja, halafu kulikuwa na Kusurura
Samweli: mashariki ya Robanda, pale unapita unakwenda Soronera
Jan : na hawa ni wa nani
George : waikumare burumarnja vilevile
Jan : kwa sasa ipo ndani park au iko wapi?
George : sehemu
Jan : mwirage iko park
Samweli: eeh
George : na Masaka iko park
Jan : haha na Bisururu?
George : Bisururu iko huku, tukienda tunawez kukuonyesha
Jan : kwahiyo hasa warumaranja walikuwa wanakaa magharibi zaidi?
George : walikuwa mashariki ya kusini

{THE END OF TAPE # 260, DONE BY NYAMUSI MAGATTI, AUGUST 2009}

261 COMPLETE

{TAPE # 261, DONE BY NYAMUSI MAGATTI, AUGUST, 2009}

{SIDE A}

Samweli: wamare wapo, warumaranja wapo, warumarunda wapo eeh hivyo hivyo
Jan: na mlipokuwa unaona watu wanavyokaa walikuwa wako ndani ya sehemu ambao sasa ni park
Samweli: kipindi kile sehemu kubwa sasa hivi ni park, nyingine imekuwa katika game reserve
Jan: mmh kwahiyo watu walisemaje wakati game pamoja na park ikaja ikawafukuza au?
Samweli: maana kwakweli hao watu wa bwana nyama wameifanya hiyo Ikoma imekuwa ndogo sana
Jan: walifanyaje?
George: walichokifanya hawakuwafukuza isipokuwa wa Ikoma wanapenda sana kuhama sasa wakihama wenyewe ile sehemu inachukuliwa

Jan: haha kwahiyo wao wenyewe wanaonawahame hivi halafu wanachukua?
George: kwa mfano ile sehemu tunayokwambia ya masaka walihama wenyewe wakaja huku wakavuka mto Romoti wakaja huku wale wakachukua, sasa sehemu ambayo wamkuja kuhamishwa kwa nguvu ni ile Mragu, walikuwa wamekataliako kabisa wakaja wakalazimika kuwaondoa
Jan: hii ilikuwa wakati gani, mwaka gani?
George: sitini na nane, sitini saba,
Samweli : sasa pale walikuwa wamebaki wachache wakawaambia tunaona afadhali muhame maana mmebaki wachache waende kule kwenye watu, sasa walijaribu kukatalia sana lakini walitumia nguvu sasa
George : hapo walitumia nguvu
Jan : na kwenda mashariki ndani ya park mwisho wa waikoma kupakana na wamaasai ilikuwa Banagi au ni wapi ambao ni mwisho wa Ikoma ndani ya park kwa mashariki sasa au Banagi walikuwa hawa ?
George : mpaka wetu na wamaasai ilikuwa mto Warangi
Samweli : mpaka wetu ilikuwa kusini mashariki ilikuwa ni karibu na Banagi
George : unajua Samwel mpaka wetu unakuja kuwa mto wa Abikore lakini mpaka wa kwanza ni Warangi, game reserve ilikuwa inaisha Banagi eeh
Jan : lakini nani waliishi Banagi ?
George: game reserve
Jan: lakini waikoma walikuwa wameishi pale zamani?
George: zamani eeh ndio
Jan: ni akina nani kwa wa Ikoma ni urumaranja ni akina nani au hii ni zamani sana?
George: {kilugha} walikuwa wanaishi hapo warumaranja
Samweli: mpaka walikuwa wanasogea hapo wanahama wanasogea kuja magharibi
Jan: haha na sababu ya kusogea ni wamaasai ni ya njaa ni kitu gani iliwatoa pale polepole?
George: eeh kitu kilichokuwa kinawatoa pale polepole wanahama hasa wamaasai eeh vita vyao ilikuwa kubwa
Samweli: vita ikiwa kali wakasogea karibu wakae pamoja wapate nguvu ya kupigana
Jan: haha sasa baba alikuwa anawasimulia ile ya jinsi walivyopigana na wamaasai?
George: eeh ndio walitusimulia
Jan: haha
Samweli: kwasababu wamaasai vita yetu na wao ilikuwa ni ng#ombe tu sasa wanaweza kuja usiku, sasa wanaweza kuja wengi sasa wakija usiku wanaingia kwenye mji kama hapa wanakuvamia wanachukua ng#ombe, wanaweza wakachukua ng#ombe mji huu, mji huu, karibu miji yote wanachukua
George: {kilugha}
Samweli: Ikoma tu#{kilugha}walikuwa wao wakija hasa wa Ikoma walipungua sana kwa ajili ya wamaasai, walikuwa wanakuja wanachoma nyumba, wanaua watu hata watoto wanaua, akina mama, wanachukua ng#ombe sasa wakishachukua ng#ombe hao wanatoka wanakwenda kupigana sana
A: wanaume wakishasikia wamaasai wameingia basi wanapiga yowe sasa watoto hawa na akina mama wanakimbia wanakwenda kujificha kwenye vichaka sasa wale wanaume

wanakwenda kupigana vita na wamaasai kuwanyang#anya ng#ombe na baadhi ya wamaasai wengine wakifika kichakani wakikuta akina mama na watoto wanajificha basi walikuwa wanaua
George: {kilugha} nilikuwa wanahelimisha juu ya wamaasai walikuwa wanakuja mchana sasa siku walikuja mchana wakaja wengi
A: walikuwa wao wametushambulia sana wakaenda wakaamua sasa twende tuwafukuze kabisa tuishi pale
Jan: hii ilikuwa lini?
George: hatukumbuki mwaka
Jan: mlikuwa ninyi mlikuwepo?
George: hapana tulikuwa hatujazaliwa, ni kati ya miaka hata baba zetu walikuwa hawajazaliwa
Jan: haha kwahiyo wakawafukuza kabisa?
George: inawezekana ikawa kati mwaka 1820
Samweli: wakati ya karne ya kumi na nane
George: kwasababu wazee wetu hata hawa babu zetu hawakupigana nao walihadisiwa
Jan: akina babu?
George: eeh babu zetu waliambiwa, halafu na ndio wakawa wanawaambia baba zetu eeh kwahiyo wao hawakupigana, waliishi kabisa , walikuja na ngozi za kukalia ili wakimaliza kuwamaliza basi wanakaa lakini wa Ikoma waliwashinda, waliwaua wengi sana
Samweli: wakauwawa wengi sana
George: tangu hapo wamaasai sasa hawakuja kupigana vita tena, kwahiyo wakaenda wakakaa chini sasa wakasema hapana tuache hawa wa Ikoma, sasa walikuwa wanakuja ni kuiba tu mpaka leo, tangu hapo vita haikuweza kupigana tena, wanaita vita ya mchana ya wamaasai na wa Ikoma
Jan: ilikuwa wajerumani bado kufika?
George: walikuwa hawajafika, wajerumani walikuwa bado hawajafika
Samweli: wanasema ni karne ya kumi na nane, wajerumani wao wamekuja mwaka gani, kumi na nne ndio wajerumani wameanza kuja
Samweli: wameanza kujenga Foti, kumi na nne ndio vita imeanza, walikuja kabla ya kumi na nne walikuja kama kumi na nane hivi
George: kumi na nane hapana, ukifika kumi na nane unarudi nyuma, kati ya kumi
Samweli: elfu moja mia nane na kitu, maana walikuja wakajenga pale Foti wakakaa, hiyo vita ya kumi na nne walikuwa wameshakaa
George: sasa muingereza wanataka kuwaondoa
Jan: mmh na wajerumani walipigana na wamaasai pia?
George: hapana
Jan: haha hawakusaidia wa Ikoma kupigana na?
George: hawakuwepo kwanza
Jan: aah wakati walikuwepo?
Samweli: wajerumani walikaa pale kikosi tu cha jeshi
Jan: ya kufanya nini?
Samweli: ya kulinda nchi
George: kulinda utawala wao, lakini swala la wamaasai wametuibia ng#ombe ilikuwa ni swala letu sisi wenyewe hawakuhusika ni sisi na wamaasai
Samweli: unajua kikosi cha jeshi hakihusiki na mambo haya ya utawala

Jan: haha kwahiyo kwanini walichagua mahali?
Samweli: Foti walipachagua kwasababu palikuwa katikati na palikuwa pazuri, plaikuwepo eneo zuri la mwinuko, walipachagua hapo kuweka kikosi cha jeshi
Jan: haha kumbi
Samweli: makao makuu ya wajerumani ilikuwa Mwanza, D.C alikuwa Musoma, hapa ilikuwa ni kikosi cha jeshi, kama vile Kiabakari
George: na sababu kubwa wao wa Ikoma walikuwepo ng#ambo hiyo walikuwepo wa Nata, eeh walikuwepo wanata na wa Isenye, wa Isenye nao walikuwa ng#ambo hiyo, kesho tukiwa tunaenda nitakuonyesha waisenye walikuwa wanakaa wapi
Jan: haha sawasawa
George: sasa pale waliona ilikuwa mwinuko mzuri na ni katikati sasa wanakaa hapo, na mawasiliano yao yalikuwa yanaenda Mwanza
Jan: na wamaasai wakati na wao walipopata njaa waliweza kuhemea Ikoma au hapana?
Samweli: wamaasai wao kazi yao ni kula nyama
George: kuenea kwao wakati wanapata njaa ndio ilikuwa wizi sasa inazidi, ndio sasa walikuwa wanatunyang#anya ng#ombe kwasababu sasa kulikuwa kuna njaa, eeh hawana namna sasa wanakuja kutunyang#anya ng#ombe, walikuwa hawali hiki chakula cha ugali wao ni maziwa na nyama na damu
Jan: na kuna kipindi ambacho ng#ombe wao wengi wakauwawa na ugonjwa Fulani, maradhi uliwahi kusikia na wao wakapata shida sana labda ni wakati wa?
George: inawezekana sasa wakati ule ndio sasa wakaamua kuja kutunyang#anya ng#ombe
Samweli: hatukuwa tunawasiliana nao
Jan: hakuna mawasiliano?
George: adui na adui
Samweli: sisi tulikuwa hatuendi umaasaini wao ni kuja hapa na kuiba, kwahiyo mawasiliano kulikuwa hakuna
Jan: na mlikuwa na mawasiliano na abasi?
Samweli: eeh wandorobo hao tulikuwa na mawasiliano nao
Jan: haha lakini ni kama wamaasai au hapana?
Samweli: ni kama wamaasai lakini jamii, yao ni kabila lao ni tofauti
Jan: kwahiyo mlikuwa na mawasiliano gani nao?
Samweli: wale walikuwa tunajaribu kufanya nao biashara kidogo na wao, walikuwa wanapata marafiki na baadhi ya waikoma, wale wakoma walikuwa wawindaji sana, walikuwa wanakutana kwa mawindo, sasa wakishakutana kwa mawindo basi wanafanyiana urafiki sasa wanaweza wakawakaribisha wakasema njooni nyumbani basi wanakuja, lakini walipokuwa wanakuja walikuwa wanakuja na biashara ya kuuziana meno ya tembo, ndio wa Ikoma walikuwa wanakata wanachezea ngoma halafu na hizi ngozi ya simba, simba mwenye manyoya makubwa, walikuwa wanakuja wanatuuzia labda tunawapa mbuzi moja au wawili ndio biashara waliokuwa wanatufanyia
Jan: haha wao walikuwa wanafuga mbuzi?
George: {kilugha}
Samweli: wale mbuzi walikuwa wanakula, mbuzi wane, watano
Jan: sio kwamba wanafuga?
Samweli: hapana, maisha yao ilikuwa porini porini tu, kuwinda tu, makambi ya kuwinda porini

Jan: na mliona jamaa yao au ni wanaume tu mnawaona?
Samweli : mimi sikuwahi kuona wanawake isipokuwa niliwahi kuona wanaume tu huko mzee moja tulikuwa jirani naye, alikuwa rafiki nilipokuwa mdogo wakaja yule mzee akamchinjia mbuzi
George: {kilugha}
Samweli: wakaja kwa mzee moja walikuwa kama wane au watano, akawachinjia mbuzi wakala basi labda wanaleta vile vitu wanauza wanarudi tena porini
Jan: wao walikuwa wanakaa wapi?
George: porini, kwenye mbuga mbuga
Jan: walikuwa na sehemu yao maalum au?
A: walikuwa wanakaa kwenye majabari, Loliondo huko kwenye majabari mpaka sasa wanaita waasi, sasa majabari hayo yako kwenye hifadhi sasa, sasa hivi hawapo
Jan: hawapo kwenye hifadhi tena?
A: wamehamia kwenye sehemu za wamaasai
Jan: na nyumba zao zilifanana na nini au hamkuwahi kuona?
A: majabari
Jan: ambayo ni kama nyasi au?
George: mawe
Jan: mawe mawe haha
George: kama jiwe kama hilo ndio walikuwa wanakaa, wanatengeza pale
Jan: na hakuna ukoo wa Ikoma ambao kwa asili yao wametokana na waasi zamani hakuna?
George: hakuna
Jan: haha walikuwa tofauti nao kabisa tangu zamani?
A: eeh walikuwa tofauti
Jan: kama wagikwe?
Samweli: aah wagikwe ni wa Ikoma, ni kusema tu ni waasi
Jan: mmh hii kusema tu?
A: ni kusema tu
Jan: ni maneno tu?
George: {kilugha}
A: ni kwasababu gani wale watu nao milango hii ilikuwa milango kuliko wa Ikoma wengine, wagaikwe na mrundi walikuwa ni wawindaji sana kuliko wa Ikoma wengine kwahiyo wao ndio maana nimesema wagaikwe walikuwa wanapenda sana kuwinda ndio wakaanza kufanya urafiki nao, maana walikuwa wanakutana porini wanashikana urafiki basi kama wana ile meno ya tembo au ngozi ya simba basi wanakuja kuwauzia
Jan: kwahiyo wakaanza kujitapia tu kwamba mimi ni mwaasi?
A: eeh mimi ni mwaasi kutokana na ile ushujaa wa kuwinda au kuua wale matembo na kuua wale masimba basi wakawa hivyo
Jan: haha na hawa wagaikwe wa Ikoma wana ukoo na wagikwe wanata au ni kitu tofauti maana naona ukoo zina kila kama Mwanchu unapata kwa Nata unapata wa Ikoma, kwa wagaikwe unapata sehemu zote mbili?
Samweli: wagaikwe wanata jamii yao wana wa Ikoma asili
George: wanata ni jamii ya wa Ikizu {kilugha}
Jan: kwahiyo ikatokeaje kwamba hivi jina la ukoo inafanana Mwancha, gaikwe kila sehemu unaipatapata

A: hata kurya wanapatikana
George: hiyo inaonekana kwamba labda sehemu za huko nyuma huko inawezekana watu hao walikuwa wa aina moja kwasababu ukienda hata kurya unakuta wako waeregi, warachi vilevile wapo, wanchage, wagikwe
A: kwahiyo inawezekana miaka nyuma zile koo zilikuwa zipo pamoja
Jan: haha na mtu ambaye ni muikoma anatambua mtu wa ukoo wa jina ile ukuryani kama ni jamaa yake au hatambui hivyo?
George: si rahisi kwavile ni mbali
Jan: kwahiyo akienda kuhemea huko ukuryani anaweza kusema wewe ni jamaa wangu?
George: eeh zamani walipokuwa wanakwena kuenea walikuwa wanachukua urafiki kwa njia hiyo
Jan: kwa njia hiyo ya kuona ukoo?
George: kwa njia hiyo sisi tunaenda kwao kwahiyo wanasema inchage kwahiyo inchage kama ni chungu {kilugha}
Jan: na walikaribishwa vizuri?
George: eeh
Jan: haha ukisema mimi nimetoka ukoo Fulani ninafanana yako?
George: eeh
Jan: sisi ndugu
George: hata hao wanaosikia waeregi ndio walikubali wao
A: unakaribishwa vizuri sana
Jan: wanakupa chakula bure?
George: eeh walikuwa wanapata chakula, ni hali ya sasa imeleta shida lakini kutokea huko nyuma kwenye chakula ulikuwa unapewa chakula, na unapewa kingine zaidi ya kile ulichonunua
Jan: haha kwahiyo ukienda kuhemea unachagua sasa naenda kwa yule ambaye unajua ana ukoo na mimi?
A: tukienda kule labda sisi watu watano, na huyu ana rafiki yake sasa tunakwenda kwa yule rafikitukishafika pale huyu anatutambulisha, kuna chakula labda ya kununua, mnasambaa mnaenda kununua sasa hapo hapo tena sisi tunapata marafiki
Jan: haha kwahiyo urafiki ni nzito kuliko ukoo?
A: eeh ukishafanya urafiki mwisho wake unakuja kujitambulisha sasa unasahu huyu ni mtu wa kwetu
George: wakati ya wale mliokwenda mkishafika kule ukisambaa kwenye kijiji sasa wanajua wageni wamekuja kwa Fulani, watu wanapokuja kuwatizama anasema wewe utakuwa rafiki yangu njoo twende kwangu, ndivyo urafiki ulivyokuwa unasambaa
Jan: haha kumbe na ile ukoo na Sonjo bado ipo au hii ni ya zamani sana?
Samweli: ni ya zamani lakini uhusiano wetu ni mazuri sana mpaka sasa ukifika kule wanaona kama ni mtu wa nyumbani, na msonjo akija huku unamwona ni kama mtu wa nyumbani
Jan: mmh na ni kama ile ya ukoo ambayo ni mbali sana lakini bado unatambuana kidogo?
George: eeh tunatambuana, wanasema ni wa kwetu hawa
A: wanasema tulitokea huko , na wao wanasema hawa ni ndgugu zetu walitoka kwetu kwahiyo bado tunatambuana

George: na ukifika pale kuna alama hapa, ukifika hapo kama wewe ni wa huku wanakuuliza hebu tuone alama yako, unatoa nguo na wanasema ni wa kwetu, hiyo alama ndio wanaona
Jan: na bado watoto wadogo wanapata?
George: eeh kwa sasa hivi sio rahisi, watoto wetu hawa wameacha, maana ile ilikuwa ni lazima kwamba kila mtoto anapozaliwa anapokuwa labda anaugua hata kama hakuugua lazima utoe hiyo nyama, walikuwa wanasema kuna nyama hapa ya mafuta, lakini sasa hivi utalaam ambao umeingia wanasema si hiyo inayosababisha ni kitu kingine
Jan: haha
George: elimu imeanza kuingia
Jan: na ile njaa kubwa ambao watu walienda ndipo walipata Machaba ni ile ya vita ya magoro hata kabla ya hiyo?
A: aah hiyo historia ya Machaba ni mbali
George: ilikuwa ni kabla na hata wakati huo walipokuwa wanapata njaa hiyo sana inabidi wafanye mitambiko ya kuwakutanisha hawa Machaba kwahiyo ni kabla, walikuwa wanasema watu walikuwa ni wachache sana ambao walikuwa wachache walikuwa wa Isenye wa waikoma sasa wakapatikana waende kutafuta ramli na uganga ili waje kuongezeka wasaidiwe ndio sasa wakaenda huko crater Ngorongoro kupita huko sehemu za Manyara
Jan: kwa watataru?
George: eeh kwa watataru ndio wanasema mtaturu, jina Machaba ya mtaturu ndio aliowapa ndio akaitwa Machaba
Jan: lakini ilikuwa watu wakati wa njaa walienda kupata Machaba?
George: eeh ndio baada ya shida kubwa sana ikabidi waende
Jan: lakini ile geti ya Magoro walikuwa wanatumia Machaba?
George: eeh walikuwa wanatumia Machaba, si yalikuwa majina mawili wanaita Ngorisa na Rogoro sasa wanayakutanisha wanayaomba walifanya kama mitambiko ya kuwaomba kwamba tunawakutanisha mme na mke sasa mtusaidie tumepata tabu, labda wapate mvua chakula, ndio imani yao
Jan: kwahiyo kila mara walipopata njaa wakafanya hii mitambiko?
George: wakafanya hii mitambiko na hata wakati ambao hakuna njaa wazee walikuwa wanasema tumechukua mtu tumewakutanisha sasa
Jan: haha pia walikuwa na mgimba wengine ambao walienda nao wakipata?
George: wagimba walikuwa ni hao watataru, wa Ikoma hawakuwa na mgimba
Jan: na watataru walikuwa wanakaa wapi?
George: wengine walikuwa wanakaa zamani sana walikuwa wanakaa hapo milima hii ilikuwa inaitwa Nyangi
Jan: haha
George: alikuwa mtaturu moja alikuwa anaitwa Zambarero anakaa hapo
Jan: alikuwa mgimba?
George: eeh alikuwa mgimba mganga, nabii yao, kwa lugha nzuri alikuwa nabii yao alikuwa anatabiri mambo yote, mambo ya biashara au vita
Jan: ilikuwa wakati gani ambayo alikuwepo?
George: eeeh#
A: miaka ya nyuma
Jan: wakati wa babu?

George: hiyo ilikuwa kwenye, wakati wa babu alikuwepo mwingine lakini Zambareko ilikuwa wakati wa mkoloni miaka ya mia tisa na moja au na mbili na tano kitu kama hicho, ndio mjerumani alikuwa anawaharakisha wafanye kazi sasa walikwenda kumwambia kwamba tumekuja kwako tumepata tabu sana na wajerumani wanatulazimisha kufanya kazi sasa tumekuja kuomba dawa
Jan: haha
George: ili tusifanye kazi, mjerumani amekuwa mkali {kilugha} sasa akaenda akawaambia hivi akawaambia mmekuja kutafuta dawa eeh nitawapa dawa lakini ngoja niwaambie dawa kubwa dawa kubwa muende mfanye kazi, mkifanya kazi mtaelewana lakini msipofanya kazi hakuna dawa, dawa ni kazi
A: basi wakaja wakajitolea wakaja wakafanya kazi
Jan: kumbe..

{END OF SIDE A}

{SIDE B}

Samweli: wanataka wakate miti, wabebe wajenge
Jan: mmh
Samweli: sasa wanasema tutafute dawa tusijenge
George: wakati huo walikuwa wanakwenda kutafuta miti, miti mingine ilitolewa mto Warangi iko mto mrefu {kilugha}
Jan: aah kumbe kwahiyo uhusiano na wataturu ilikuwa nzuri sana?
George: eeh wataturu na wa ikoma aah sana
Jan: ni kama baba?
George: eeh ndio ni marafiki, hata ulikuwa unaenda pale unataka hata azungumze unamsogelea azungumze mate yake wanaruka yanaporomoka mengine anakutemea, kwahiyo tulikuwa tunawaabudu
Jan: haha#hata mlipokuwa nay owe kwa wamaasai waliwasaidia
George: eeh dawa zilikuwa zinasaidia, hata ile mito tunayosikia kwamba ni ya mchana waliitabiri kwamba itakuwepo wanasema walikwenda kwa wabiha muende mjiandae mtengeneze mishale kila mtu vita ipo na wanasema wamaasai watakuja kuchukua ng#ombe mchana
Jan: eeh
George: ndio aliwatabiria
Jan: na walikuwa wanakaa sehemu ile tu ambayo ulitaja au sehemu nyingine pia?
George: wa?
Jan: wataturu walikaa?
George: milima ya nyangi
Jan: kuna sehemu nyingine?
George: baadaye wakavuka mto wakawa ng#ambo huko sehemu za Sibora huko eeh walikaa hapo baadaye ndio wakaendelea kuhama kwenda {kilugha]
Samweli; {kilugha}

Jan: kuna sehemu ambazo kama lisambwa ambayo ni muhimu kwa wa Ikoma ambao bado wanaenda kutambikia pale, ni kama sehemu gani au ambao watu bado wanakumbuka site zile za muhimu muhimu ya kutambikia?
Samweli: eeh#mahali kama Maserebati
George: {kilugha}
Jan: na Marishi
George: na warangi na Marishi
Jan: mmh nini imetokea huko ambao bado wanakumbuka?
George: wao wanasema asili yao walikuwepo huko wa kwao kule kwao walipokuwa huko ndio wakaja wakashambuliwa na hawa watu wakawauwa wakahama hapo wakawasambaza, wanakwenda pale wanachinja ng#ombe wanawinda wanasherekea
George: walikuwa wanaomba hata kibali
Samweli: hata miaka hii ya karibuni walikuwepo, kuja themanini au tisini
Jan: kuna sehemu maaalum na kaburi na nini?
Samweli: eeh
George: {kilugha}
Jan: haha kuna wazee ambao bado wanakumbuka walienda wapi?
Samweli: eeh yupo mdogo wangu ambaye alikwenda, yuko Robanda
Jan: aah yuko robanda hata anaweza akaenda na sisi?
Samweli: eeh mnaweza mkaenda pale, mnapata kibali
Jan: na kuna sehemu nyingine ambayo ni maalum?
Samweli: wa Ikoma wote wana mahala, na baadaye kila mlango ina mahala pake kwa kuabudu, waikumare, wamwancha eeh
Jan: kwahiyo ni wapi ambao kila..
Samweli: abarachi {kilugha}
Jan: wanaenda wapi?
Samweli: kuna mlima Robanda, mlima huo mkono wa kushoto
Jan: inaitwaje?
Samweli: Nyabati ndio walikuwa wanakwenda, kuna sehemu wale warachi walikuwa wanaabudu nyoka chafu ilikuwa inakaa hapo, sasa walikuwa wakipata shida ule mlango ule unakwenda unachukua mbuzi mweupe dume basi wanapandisha kule na akina mama wanachukua kuni wanachukua na chakula wanapanda wanakwenda wanashinda pale siku nzima, wanachinja yule mbuzi pale wanapika chakula pale wanakula sasa labda jioni labda saa kumi ndio wanateremka sasa
George: eeh na wakifik pale wakikaribia wanavua viatu
Samweli: kama hapa na nyumba ile basi wanavua viatu, sasa wanakwenda wanakaa wanachinja yule mbuzi na akina mama wanapika
George: halafu wanaenda watu watakaoenda pale ni wale watakatifu hasa
Samweli: sio watu wenye dhambi
George: kama wewe umekosa karibuni wewe huwezi kwenda, halafu kama mama yuko mwezini au akina mama wote ambao wanajua wako hivyo hawaendi
Jan: mmh sawasawa
George: maana ana madhambi, lazima awe kulikuwa na sehemu moja inaitwa egesima yani kisima, chemchem Fulani wanasema kwamba kuna Kumare anakaa pale, sasa walikuwa

wanakwenda kuabudu hapo hata wakati mvua zimekosekana wanakwenda pale, wanachimba, na watu wanaenda pale wa aina hiyo, wakikaribia pale wanavua viatu, halafu wanajipeleleza nani ambaye hali yake si nzuri, mwenye makosa makosa hatakiwi
Jan: aah kumbe
George: wakienda wasipofaulu siku hiyo wakienda labda kama mvua haiwezi kunyesha wanajiuliza nani alikuwa mbaya kule, alikuwa na shida ambaye anasababisha maombi yetu yasisisike eeh kwahiyo ilikuwa ni mtakaso wa hali ya juu
Jan: mmh kumbe sawasawa na hizi site nyingi ya hizo ipo nje ya park au iko ndani?
George: sehemu hizi tunazozungumza za mwisho hizi iko labda hii ya huku juu, yam lima ipo hapo kijijini
Samweli: nah ii nyingine ya kisima hii sina hakika kama ipo ndani
George: aah ipo ndani ya game reserve
Jan: na huko Banagi ina lisambwa yake au hii ilikuwa?
Samweli: isipokuwa hii tunayosema iko chini ya national park
George: {kilugha}
Samweli: {kilugha]
George: kuna sehemu moja vilevile ilikuwa inaitwa embe na kamlima Fulani ilikuwa inaitwa ebo walikuwa wanakaa
Jan: iko wapi?
George: iko chini mwa Robanda, national park
Samweli: {kilugha}
George: {kilugha}
Jan: kwahiyo wa Ikoma nah ii game pamoja na hii national park walikuwa na uhusiano gani?
Samweli: hao mara ya kwanza watu walionza kuingia pale ni hawa wananyama hawa wa game
George: game ndio ilianza
Jan: na ilikuwa shamba la bibi?
George: eeh game ndio ilikuwa, ndio ilikuwa inakaa Banagi wanasema inachunga shamba la bibi
Samweli: watu walioanza kuandikwa kazi ni wa Ikoma, ndio walikuwa askari ndio walikuwa karibu
Jan: kwahiyo uhusiano ulikuwa mbaya au mzuri?
Samweli: ulikuwa mzuri tu haukuwa mbaya sana, hawakuwa wakali zaidi
Jan: si waliwazuia msiwinde?
George: haha walikuwa wanazuia wasiingie kwenye shamba la bibi
Jan: aah ok
George: huko ndani tulikuwa tunawinda
Jan: haha kwahiyo hawana shida kama unawinda huko?
George: hawana shida ili mradi usiingie kwenye shamba la bibi
Jan: ukiwaona unabeba nyama nje ya game?
George: aah hamna shida
Jan: aah
George: wao si wanakaa banagi wala hawaji kutafuta watu, ndio walikuwa wanakatalia shamba la bibi
Jan: aah

George: unajua hili shamba la bibi limeanza baada ya muingereza kutawala
Samweli: eeh ilikuwa Ritoya
George: na aliyetawala aliyekuwa queen ni nani?
Jan: aah queen
George: kingi mke wake anaitwa nani?
Jan: si ni queen
George: siyo ilikuwa shamba la queen
Jan: sawa kwahiyo wakati walianza kuzuia watu wasiwinde kabisa ni kipindi gani?
George: ni miaka hii ya karibuni
Jan: wakati wa national park ilipoanza?
Samweli: {kilugha} wakati tunaanza kusogeza mipaka sasa national park inaanza kuingia
George: national park ilianza kuingia kwenye mwaka hamsini, hamsini na mojan a mbili tulipoanza kudai uhuru sasa ndio wakataka kupanua mipaka sasa wakati huo ndio tulikuwa na madiwani sasa chief Nyahoche maana miaka ya hamsini na sita n asaba na nane hapo ndio walikuwa wanakuja sasa tunakumbuka alikuja judge Wambura na mhindi moja tukatoka pale mpaka mangwesi sasa wanadai kuongeza mpaka ndio tukakubaliana sasa wakatoka mpaka kwa Warangi tukaja Bomoko
Samweli: {kilugha}
George: {kilugha} ni hatari {kilugha} ni hatari ilikuwa
Samweli: sitini na sita
Jan: sitini na sita ikafanyaje?
George: aah hiyo ni ya hapa
Samweli: walikuja national park wakalima hapa kwenye mashamba
George: aah walikuja ile sehemu waliona kwamba wakati wa utawala wa mwalimu Nyerere wanakaa pale national park hawalimi, wake zao hawalimi wakasema waje tuwape shamba hapa walime ili wapate chakula wavune wapereke huko kwao
Jan: aaah
George: kule Soronera
Jan: haha
Samweli: baadaye wakaona kazi mbili kulima na kazi ya kuchunga wanyama watashindwa wakachagua ya wanyama, wakalima mwaka mmoja tu
Jan: haha kumbe kwahiyo baada ya park kuuingia wakaanza kuzuia watu wasiwinde?
George: ndio sasa park ilipoingia pale kwenye miaka hiyo tunayoyasema basi game reserve nayo ikabadilika ikawa ni ndani ya wananchi sasa, mmh game reserve sasa wakaanza kukatalia wanyama hata kwenye national park haingii kwenye miji kutafuta wanyama lakini game reserve inaingia kwenye miji kwasababu wanakaa karibu na raia maanake ni kwamba wananchi wamekaa kwenye game reserve
Jan: haha mnavyoona sasa hivi hii watu wa huko hifadhi wameanza kuwa na uhusiano mzuri na watu au bado ni kama wanagombana nao?
George: bado mahusiano yao ni kidogo
Samweli: ingawa yapo kiasi lakini ni kidogo, lakini wanawapa msaada na hospitali wamewajengea
George: lakini bado mahusiano si kamili sana

Samweli: wanawafinya sana wananchi, maeneo yamefinywa yamekuwa madogo sana hata wananchi hawapanuki
George: sasa kinacholeta mahusiano kuwa mabaya ni nchi, wanawabana sana, ile kuhama ya zamani wa Ikoma walikuwa wanahamahama sasa imeisha sasa hii ndio wanachukia sana
Samweli: sasa huwezi kwenda sehemu nyingine sasa hata kama unapenda kusogea sasa huwezi wanasema hapa ndio mpaka sasa huwezi kuja hapa na wewe labda wewe unapenda kusogea na kufunga mifugo na kulima mashamba wanasema aah hapa huwezi kulima na hapa huwezi kufunga mifugo sasa mnabanana tu sasa hiyo wananchi hawapendi, hata pale Robanda ni pafinyu sana, watu wanabanana tu
Jan: na huko Robanda kuna hii nasikia sengo, safari kuna hawa makampuni ya nje wanakuja na watalii hii ni mabo mazuri kwa wa Ikoma au inaharibu zaidi?
George: ni kwamba kwa makutano ya sasa waliyo nayo kama itakuwa hivyo yatakuwa mazuri lakini kuna mashaka kama itaendelea kuwa mazuri maana inawezekana baadaye maana mtu kuingia ni rahisi, mkataba wanasema ni muda mfupi lakini inawezekana wakaona utamu wakaongeza baadaye wakachukua mipaka, hata JD inaanza kuleta utata Nata kwasababu waliwapa maneno ya haraka haraka na nini watu wakafikiri ni kweli wakaandishikana mkataba ya miaka tisini na tisa, sasa wamekuja kugundua tumeweka mkataba sasa watoto wetu watakuwa wanaishi wapi eeh kwahiyo inaanza kuleta utata
Jan: kwahiyo wakawapa mkataba ya miaka tisini na tisa bila kuwaambia watu wazi?
George: eeh pale JD pila kuwaelemisha watu, waliwahidi watawatengenezea hiki, watawapa hiki, unajua mtu kama anataka kuingia wewe kama ni masikini huna chochote anaweza akakwambia kila siku nitakuwa nakuletea kilo ya sukari ukafikiri ni kweli ukasaini mkataba ukajifunga, sasa wanata wameanza kusema na barabara hii ya huku iame sasa inaleta shida, sasa hivi wako kwenye shida hawaelewani ndio maana yule mzungu kutoelewana na yule wa kwanza ndiyo akahama akauza hiyo akamuuzia huyu
Jan: na eneo ni kubwa?
George: eeh eneo ni kubwa
Samweli: lakini kulingana na eneo aliyokuwa amepewa yule sasa huyu tena anataka achukue sehemu ya game tena, sasa hii imeleta ukorofi
George: bado anaona ni ndogo anataka apanue sasa hiyo na wanata wanasema hapana, hiyo inaleta shida
Jan: mmh na hawa wa Robanda wako vilevile au?
George: hata wa Robanda wako kwenye hali hiyohiyo ingawa haijajitokeza lakini mashaka yapo, watu wanaanza kuhoji maswali
Samweli: maana maeneo yale pale yalikuwa ni miji
Jan: lakini mpaka sasa wanakaa kama jirani mwema?
George: eeh wale sasa hawana shida
Jan: hawana shida?
George: lakini kuna mashaka
Jan: ya mbali?
Samweli: kwasababu watu, hata Robanda yenyewe hasa miaka ya kuanzia miaka ya sitini na tatu ilikuwa ni kidogo sasa hivi imeeanza kupanuka, watu wanaleta ukorofi watu wanataka kujenga wanataka kulima sasa ukiwaambia waondoke na mkataba wake ule haujaisha si watagombana

Jan: eeh ndio watagombana
Samweli: eeh
Jan: na nyinyi mnavyoona hii wanyama pori wangeisha bila kuhifadhiwa na hawa wa game au haina shida?
Samweli: kwa sasa tunaona kuna hatari game kuwepo inasaidia na national park inasaidia maana sasa hivi wanyama wanaingia kwenye biashara
George: tofauti na wa Ikoma wa zamani tulikuwa tunawinda ya mboga tu
Samweli: tunapata nyama kidogo, labda nyama kilo ishirini thelathini unauza tu kwa kitu kidogo lakini sasa hivi wanafanya magunia na lori wanauza mpaka Kenya, sasa unauza hata magunia kumi sasa ni hatari wanyama kuisha kwahiyo hilo tuliona ni zuri maana bila hilo wanyama wataisha#
Jan: mmh lakini watu ambao wako hapa wangekuwa na uhuru wa kuwinda hata kidogo au itakuwa inaisha kabisa?
Samweli: sisi uwindaji wetu haikuwa na zana kali kama ya saa hivi uwindaji wa mishale nah ii ya kuchimba shimo unaua wanyama watatu wane au watano lakini sasa unakuta watu wameua wanyama hata thelathini mtu anakwenda anakaa wiki moja au wiki mbili watu wengi zaidi ya ishirini wanaua wanyama wengi sana sasa ukifanya kwa muda wa miaka mingi wanyama watakwisha kwahiyo hiyo tunaona hiyo ni nzuri sana kwasababu sasa hivi spidi ya kuwinda ni kali sana
Jan: wangeweza kuzuia ile ya biashara na kuacha watu wa kawaida
Samweli: eeh watu wa kawaida wanapata mboga
Jan: haha lakini hii kwa leo haipo ya kwenda kupata mboga wako?
Samweli: haipo wanakataa kabisa isipokuwa kama Robanda pale ndio kuna wanyama wachache
George: wanakuja kuuzia wananchi
Samweli: wanawauzi wananchi
George: {kilugha}
Jan: nyie mna ushauri gani katika hii maneno ya uwindaji?
Samweli: tulikuwa tunafikiri game wangepatia wananchi wawe wanapata mboga kwasababu sisi tulishazoea, sisi ni wawindaji tangu asilia sasa tulikuwa tunafikiri game wangetupa nafasi huwa tunapata mboga, sisi tunapenda mboga za porini
Jan: kuwinda wenyewe
Samweli: eeh kuwinda wenyewe
Jan: na upinde au lazima iwe bunduki?
Samweli: hata kwa bunduki, siku hizi watu wengi wana bunduki, tunapata nyama za porini cha mboga hiyo ingekuwa ni vizuri lakini kuzuia kabisa kabisa tutakuwa tumepoteza kidogo tunabanwa sana na mboga tunapenda, sasa kila siku tutakula mboga za majani vilevile lakini kama majira haya mboga zinapatikana tungeshauri iwe hivyo, lakini kukataa kabisa kabisa tulishazoea tangu babu zetu tutakuwa kidogo tunanyimwa uhuru
George: halafu vilevile kuongezea hilo ni kwamba wengine wanaotuzia kuingia national park, sisi kama wenyeji wa hapa turuhusiwe kuingia kule maana ndio sehemu yetu ya asili sasa wanapotuzuia tusiingie mpaka tulipe malipo basi wanatuumiza, sisi ndio wenyeji wa hapa sasa tunafaidika na nini kama wenyeji wa hapa wa asili ya hapa tunafaidika na nini
Jan: eeh ndiyo

Samweli: tumebanwa kidogo
George: tunaingia tunapatembelea, kama wenyeji wa Ngorongoro hawalipi kitu chochote wanaingia tu
Jan: aah wanakaa ndani
George: wanakaa ndani
Jan: unaposema kwamba asili yenu ni uwindaji ni pamoja na kilimo na ufugaji au hii ilitangulia?
George: vyote vitatu
Samweli: zinakwenda kwa majira, uwindaji tunapenda kuwinda mwezi wa sita mpaka mwezi wa kumi na moja wanyama wanaweza kutoweka kabisa wanaenda mashariki sisi tunabaki kulima na mifugo, tunakuwa na kazi mbili kulima na kufuga, kwahiyo tunakwenda kwa majira, mpaka mwezi wa sita tena, mwezi wa tatu tunakoma kulima sasa tunafuga na tunavuna ndio sasa ndio tunaanza kulima sasa, kwahiyo ile ni ya muda, uwindaji ni yamuda lakini kilimo nacho ni cha muda vilevile lakini ufugani ndio muda wote
Jan: na mashamba ya kilimo yalikuwa karibu na nyumba au ni mbali?
Samweli: watu wanalima mbali, tulikuwa tunalima mbali zamani, zamani tulikuwa tunatoka Robanda pale tunakwenda kulima kule mto wa rangi na wengine wanakuja kulima Foti na wengine wanakwena mashariki
George: tulikuwa tunaweza kwenda kulima kilomita kumi mpaka kumi na tano mpaka ishirini
Samweli: na watu wanahamia kule wanajenga nyumba hukohuko wanakaa mpaka wanavuna
Jan: kwanini waliamua kulima mbali sana?
Samweli: walikuwa wanategea mvua eeh kule#

{THE END OF TAPE # 261, DONE BY NYAMUSI MAGATTI, AUGUST 2009}